Je, Mwalimu wa Family Day Care ni nani?

SWAHILI

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:

Je, Mwalimu wa Family Day Care ni nani?

Mwalimu wa Family Day Care ni mtu anayetoa huduma za masomo ya utotoni yaliyoidhinishwa na kutunza watoto (hususan watoto wadogo ambao bado hawajaanza kuenda shule) katika nyumba ya mwalimu huyo.

Huduma za Family Day Care zimekuwa zikiendelea nchini Australia kwa zaidi ya miaka 40. Familia husajili watoto wao katika Family Day Care wanapokuwa wanafanya kazi, kwenye mafunzo au wanasoma.

Walimu wa Family Day Care hutoa huduma za elimu ya utotoni iliyoidhinishwa na hutunza watoto katika mazingira ya kinyumbani

Kuwa Mwalimu wa Family Day Care kunaweza kuwa njia nzuri ya mapato. Unaweza kuthibiti maisha yako ya kazi huku ukitunza na kusomesha watoto katika nyumba yako. Utakuwa pia unasaidia familia za watoto hao ili zishughulikie mambo mengine kama vile kazi na masomo.

Kama Mwalimu wa Family Day Care, unaweza kutunza hadi watoto saba (wakiwemo watoto wako mwenyewe walio chini ya umri wa miaka 13) lakini watoto walio na umri wa shule ya chekechea au mdogo zaidi wasizidi wanne.

Utunzaji wa watoto ni kazi muhimu. Unaweza kuleta mabadiliko katika maisha yao kwa kutoa huduma ya utunzaji bora na kuwafundisha vizuri katika mazingira salama.

Walimu wa Family Day Care hufanya kazi nyingi zaidi ya kucheza na watoto tu. Huwasaidia watoto katika masomo kupitia michezo mbali mbali wanayotoa na pia wana jukumu la afya na uzima wa kila mtoto wanayemtunza.

Walimu wa Family Day Care wameunganishwa na familia kupitia huduma ya Family Day Care

Kwa sababu kutunza watoto ni kazi muhimu sana, unapoamua kuwa Mwalimu wa Family Day Care, ni lazima kwanza ujiunge na huduma iliyoidhinishwa ya Family Day Care. Huduma ya Family Day Care itakupa usaidizi na mafunzo na kupendekeza huduma zako kwa wazazi. Pia watakagua jinsi unavyowaangalia na kutunza watoto walio chini ya uangalizi wako. Wao pia hupokea ada kutoka kwa wazazi na kisha wanakulipa. Vile vile hutoa usaidizi wa Serikali ya Australia wa ada za utunzaji wa watoto kwa niaba ya familia zinazostahiki.

Unaweza kuchagua kwa hiari ni kituo gani cha huduma ya Family Day Care ambacho unataka kujiunga nacho. Ni muhimu uchague huduma ya Family Day Care unayoamini inaweza kukusaidia na kufanya linalofaa.

Vituo vya huduma ya Family Day Care huwashirikisha walimu kama wafanyakazi au kama wakandarasi wa biashara ndogo ndogo. Kusimamia biashara ya Family Day Care ni kama kusimamia biashara yako ukiwa nyumbani.

Vituo vya huduma za Family Day Care lazima vihakikishe walimu wake wanazingatia sera na taratibu zao zote pamoja na Sheria ya Usaidizi wa Familia.

Serikali hutoa ruzuku kwa familia zinazotumia huduma zilizoidhinishwa za Family Day Care

Serikali ya Australia hutoa ruzuku kwa familia zinazostahiki na zinazotumia huduma za Family Day Care ili kusaidia kupunguza gharama ya ada ya huduma hizo. Kama Mwalimu wa Family Day Care, unahitaji kuweka rekodi sahihi za maudhurio kwa kila mtoto unayetunza, ili kuhakikisha wewe na kituo cha huduma ya Family Day Care hamvunji Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Kuna Kiwango cha Ubora cha Kitaifa cha huduma za elimu na za utunzaji

Kwa sababu ni muhimu kwa watoto kupokea elimu na huduma za utunzaji zilizo bora zaidi, kuna mfumo unaohakikisha kwamba huduma nyingi za elimu na utunzaji, ikiwa ni pamoja na Family Day Care, zinafanya kazi kuimarisha ubora wa elimu na utunzaji wanaopokea watoto. Kuna kiwango cha chini kabisa ambacho huduma zote zinajibidiisha kupita – Kiwango cha Ubora cha Kitaifa cha Huduma za Elimu na Utunzaji.

Kiwango cha Ubora cha Kitaifa husaidia walimu kuelewa jinsi ya kutoa elimu na utunzaji bora zaidi katika mazingira mazuri inavyowekezana ili kusaidia watoto kuendelea, kusoma, na kukua.

MAMBO MUHIMU YA KUTILIA MAANANI

- Walimu wa Family Day Care hutoa huduma za elimu ya utotoni iliyoidhinishwa na hutunza watoto wa watu wengine katika nyumba zao.
- Walimu wamesajiliwa na, na hufanya kazi chini ya uelekezi na usaidizi wa huduma iliyoidhinishwa ya Family Day Care.
- Huduma za Family Day Care hushirikisha walimu kama wafanyakazi au kama wakandarasi wa biashara ndogo ndogo.
- Serikali ya Australia hutoa ruzuku ya huduma za utunzaji wa watoto kwa familia zinazostahiki ili kuzisaidia kugharamia ada za huduma ya Family Day Care. Kituo cha Huduma ya Family Day Care lazima ipitishe ruzuku hizo kama punguzo za ada kwa familia ambazo zimechagua mpango huu.
- Kuwa mwalimu ni kazi yenye manufaa sana. Unaweza kuleta utofauti kwa watoto kwa kutoa huduma ya utunzaji bora na kuwafunza vizuri katika mazingira salama.
- Family Day Care inadhibitiwa sana – walimu na vituo vya huduma lazima vizingatie sheria na kanuni kadhaa ili kuhakikisha uadilifu wa ruzuku za Serikali ya Australia na kuhakikisha watoto wanatunzwa katika mazingira salama.
- Ni muhimu uelewe majukumu unayojitwika unapoamua kuwa mwalimu wa Family Day Care. Lazima utilie maanani masuala ya kifedha na kisheria – ukiwa na shaka kuhusu unachoambiwa ufanye na kituo cha huduma ya Family Day Care, uliza.
- Ikiwa unafikiri unaambiwa ufanye ulaghai au kitendo kinachovunja sheria, unaweza kupiga simu kwa laini ya kutoa habari kupitia **1800 664 231** au utume barua pepe kwa: **tipoffline@education.gov.au**
- Njia bora zaidi ya kuhakikisha kwamba unapata usaidizi katika kazi yako kama mwalimu wa Family Day Care ni kujiunga na huduma ya Family Day Care ambayo itakusaidia na unayoamini.

Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Je, nahitaji kuwa na sifa stahiki?

Unahitaji kuwa na, au uwe unaendelea kupata mafunzo ya kuhitimu kuwa na – Cheti kilichoidhinishwa cha III katika Huduma za Elimu na Utunzaji. Mafunzo haya ambayo unaweza kusoma katika chuo cha TAFE au kupitia shirika la mafunzo lililosajiliwa, yatakusaidia kuboresha ujuzi wako wa kutunza na kufunza watoto wadogo.

Nitahitaji kufanya nini kingine?

Utahitaji:

- Kuwa na kibali cha sasa cha Ukaguzi wa Kufanya Kazi na Watoto
- Kuwa umesajiliwa na kituo cha huduma ya Family Day Care. Watakuunga mkono na kukusaidia kufuatilia huduma unayotoa kwa watoto.
- Kuwa na mafunzo ya sasa ya huduma ya kwanza (ikiwa ni pamoja na Cheti cha ufahamu wa utaratibu wa dharura wa kimatibabu wa kufanya moyo uanze kupiga tena na mtu apumue (CPR) na mafunzo katika uthibiti wa dharura wa pumu na mzio).
- Kuwa na bima ya dhima ya umma
- Kushiriki katika warsha za kuendeleza taaluma yako na za mafunzo.
- Kufanya kazi na watoto kwa njia zilizoainishwa katika Kiwango cha Ubora cha Kitaifa cha elimu na utunzaji,ukitumia mtaala ulioidhinishwa.
- Kuhakikisha unafuata Sheria ya Kitaifa na kanuni na unazingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Nitapokea mshahara wa pesa ngapi?

Vituo vya huduma za Family Day Care huweka kiwango chao cha ada. Kiwango hicho cha pesa kinalingana na au ni zaidi kidogo ya kile wanachopokea walimu wanaofanya kazi katika vituo vya kutunza watoto.

Je, ni lazima niwe na nyumba yangu?

Hapana. Kama watoto wanaweza kutunzwa kwa usalama na kuwe na nafasi inayotosha, haijalishi kama nyumba ni yako au ni ya kupanga. Lakini unahitaji kudhibitisha ikiwa unahitaji ruhusa kutoka kwa wakala wako wa upangaji wa nyumba.

Je, ninaweza kutunza watoto wangapi?

Sheria inatoa mwongozo wa idadi ya watoto unaoweza kutunza. Kwa sasa, unaweza kutunza watoto saba (ikiwa ni pamoja na watoto wako walio na umri wa chini ya miaka 13) lakini watoto walio na umri wa shule ya chekechea au chini wasizidi wanne.

Je, ni sheria na kanuni gani zinazohusu Family Day Care?

Kuna sheria kadhaa zinazoelekeza jinsi huduma za Family Day Care na walimu wanapaswa kuendesha shughuli zao. Kanuni ambazo ni muhimu sana ni:

- **Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Elimu na Utunzaji**
  www.acecqa.gov.au/national-law
- **Kanuni za Kitaifa za Huduma za Elimu na Utunzaji**
  www.acecqa.gov.au/national-regulations
- **Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani**
  www.education.gov.au/family-assistance-law

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.

FAHAMU MENGI ZAIDI

Umevutiwa? Fahamu mengi zaidi kwa kutembelea tovuti zifuatazo:

- **www.education.gov.au/family-day-care**
- **www.fdcsupport.org.au**
- **www.fdca.com.au**
- **www.acecqa.gov.au**

au kwa kuenda kwa kituo cha huduma ya Family Day Care kilicho karibu nawe. (Ili kupata kituo cha huduma hii kilicho karibu sana, tembelea tovuti **www.fdca.com.au** na kisha ubofye kichupo cha “find childcare”.)